

Magonjwa yanayochunguzwa kupitia kupimwa kwa damu, yanaendelezwa:

- Hb S/C disease (Hb S/C)
- Holocarboxylase synthetase deficiency (MCD or multiple carboxylase deficiency)
- Homocystinuria (HCY)
- Isovaleric acidemia (IVA)
- Long-chain L-3-OH acyl-CoA dehydrogenase deficiency (LCHAD)
- Maple syrup urine disease (MSUD)
- Medium-chain acyl-CoA dehydrogenase deficiency (MCAD)
- Methylmalonic acidemia: cobalamin A, B (Cbl A, B)
- Methylmalonic acidemia: mutase deficiency (MUT)
- Mucopolysaccharidosis type I (MPS I)
- Phenylketonuria (PKU)
- Pompe disease
- Propionic acidemia (PROP)
- Severe combined immunodeficiency (SCID)
- Sickle cell anemia (SCA or Hb S/S)
- Spinal muscular atrophy (SMA)
- Trifunctional protein deficiency (TFP)
- Tyrosinemia type I (TYR I)
- Very long-chain acyl-CoA dehydrogenase deficiency (VLCAD)
- X-linked adrenoleukodystrophy (X-ALD)

Aina nyingine mbili za kupimwa zinafanywa katika hospitali au na wakunga:

- Critical congenital heart disease (CCHD)
- Hearing



**Maswali? Wasiliana nasi katika
800-660-4427 au 802-951-5180**



Mpango wa Vermont wa Kuchunguza Watoto Wachanga

Idara ya Afya ya Mama na Watoto
Watoto wenye Mahitaji Maalum ya Kiafya
108 Cherry Street, Sanduku la Posta 70
Burlington, VT 05402 healthvermont.gov/family/newbornscreening
800-660-4427 (Vermont pekee) au **802-951-5180**
Faksi: 802-951-1218

Ilisahihishwa 7/16/2019

Swahili

Mpango wa Vermont wa Kuchunguza Watoto Wachanga



Watoto wote wanaozaliwa Vermont wana nafasi ya kufanyiwa uchunguzi wanapozaliwa ili kukagua magonjwa nadra lakini hatari ambayo sio dhahiri wanapozaliwa.

Je, ni kwa nini mtoto wangu anahitaji kufanyiwa uchunguzi wa magonjwa anapozaliwa?

- Tunapendekeza watoto wote kufanyiwa uchunguzi wa magonjwa wanapozaliwa, hata ingawa wana afya bora.
- Kufanyiwa uchunguzi kwa watoto wanapozaliwa kunasaidia kukagua damu ya mtoto kwa matatizo ya kiafya yaliyo nadra na ambayo yanaweza kusababisha ugonjwa au kifo.
- Punde tu matatizo haya ya kiafya yanapatikana mapema kwa kupimwa, watoto wanaweza kupokea matibabu na utunzaji wanaohitaji.
- Watoto wengi wana afya nzuri wanapozaliwa lakini bado ni muhimu kuwapima.

Je, mtoto wangu atapimwa vipi?

- Mtaalamu wa huduma ya afya atachukua kiasi kidogo cha damu kutoka kwa kisigino cha mtoto na kuituma kwenye maabara.
- Mtaalamu wa afya pia atakagu matatizo ya kusikia na moyo. Kupimwa huku hakuhitaji damu yoyote.
- Wakunga wanaweza kumpima mtoto wako iwapo amezaliwa nyumbani.
- Wazazi au walezi ambao hawataki watoto wao wapimwe wanaweza kukataa kwa kutia sahihi kwenye fomu. Mtaalamu wa afya anafaa kuelezea hatari ya kukosa kupimwa kabla ya fomu kutiwa sahihi.



Je, nitayapokea vipi matokeo ya kupimwa?

- Mtaalamu wa afya wa mtoto wako atakueleza matokeo.
- Inaweza kuchukua muda wa siku chache kabla ya matokeo kuwa tayari.
- Matokeo ya kupimwa moyo na uwezo wa kusikiza yanapatikana mara moja.

Je, mbona mtoto wangu ahitaji kupimwa tena?

- Iwapo kupimwa kulifanywa kabla mtoto wako afike umri wa saa 24.
- Iwapo kuna matatizo na jinsi kupimwa kulifanyika.
- Iwapo matokeo ya kupimwa kwa kwanza yalionyesha uwezekano wa matatizo ya kiafya.

Je, nitafanya nini iwapo mtoto wangu atahitaji kupimwa tena?

- Mtaalamu wa afya wa mtoto wako au Mpango wa Kuchunguza Watoto Wachanga watawasiliana nawe iwapo mtoto wako anahitaji kupimwa tena. Watakuieleza ni kwa nini mtoto wako anahitaji kupimwa tena na ni kipi unahitaji kufanya.
- Ni muhimu kufuata maagizo ya mtaalamu wa afya na kumpeleka mtoto wako kupimwa.
- Hakikisha kwamba hospitali na mtaalamu wa afya wa mtoto wako wana anwani na nambari yako ya simu iwapo watahitaji kuwasiliana nawe kuhusu matokeo ya uchunguzi.

Je, sampuli ya damu ya mtoto wangu itafanyiwa nini?

- Katika Vermont, sampuli za damu zinahifadhiwa kwenye maabara na kuharibiwa baada ya mwaka mmoja. Sampuli inaweza kuharibiwa mapema ama kuhifadhiwa kwa muda zaidi kwa kutuma ombi lililoandikwa kwa Mpango wa Vermont wa Kuchunguza Watoto Wachanga.



Vermont mara kwa mara huchunguza watoto wachanga ili kubaini magonjwa 35. Kati ya hayo, 33, yanachunguzwa kwa kupima damu:

- 3-Methylcrotonyl-CoA carboxylase deficiency (3MCC)
- 3-OH 3-CH3 glutaric aciduria (HMG)
- Argininosuccinic acidemia (ASA)
- Beta-ketothiolase deficiency (BKT)
- Biotinidase deficiency (BIOT)
- Carnitine uptake defect (CUD)
- Citrullinemia (CIT)
- Congenital adrenal hyperplasia (CAH)
- Congenital hypothyroidism (CH)
- Cystic fibrosis (CF)
- Galactosemia (GALT)
- Glutaric acidemia type I (GA I)
- Hb S/Beta-thalassemia (Hb S/Th or Hb S/A)

yanaendelezwa upande huo mwingine

